# UNIONI MISHENI YA KUSINI MWA TANZANIA

## JUMA LA MAOMBI LA HUDUMA ZA FAMILIA

**Novemba 02 – 09, 2019**

**MADA: FAMILIA YENYE FURAHA**

**FUNGU: Wafilipi 4:4**
**“Furahini katika Bwana siku zote; tena nasema, Furahini”**

**WIMBO: “Kuwa na Yesu Nyumbani” (Na. 204)**

**Limeandaliwa na Idara ya Huduma za Familia**
**Unioni Misheni ya Kusini mwa Tanzania**

**SOMO 1** **Novemba 2, 2019**

## "NI NANI MKUU NYUMBANI KWANGU?"

### Wafilipi 4:4 "Furahini katika Bwana siku zote; tena nasema, Furahini"

**UTANGULIZI**

Kwa hiyo mume anasema "Mimi ndiye mkuu hapa nyumbani kwa sababu ninahangaika na kuleta chakula." Na mke naye anajibu kuwa, "Mimi ni shingo inayotegemeza kichwa.! Kwa hiyo mini ndiye mkuu nyumbani." Swali kubwa ni hili: "Ni nani anatakiwa kuwa mkuu katika nyumba ya Kikristo? Ni nani anayetakiwa kuwa mkuu ndani ya familia ya Mungu yenye furaha? Hebu tutumie funguo tano ili kujibu swali hili.

**KUJISALIMISHA KILA MMOJA KWA MWENZAKE**

**I. Mume ndiye kichwa cha nyumba.**

Maandiko: Waefeso 5:23 Katika mwili wa binadamu, akili inatiisha mfumo wa neva
Mfumo huo unapokea jumbe kutoka katika sehemu zote za mwili. Mfumo huo unatuma jumbe katika kila sehemu ya mwili. Jumbe hizi zinasafiri kwa kasi isiyo ya kawada. Mume kama kichwa cha nyumba anatakiwa kuwa mlinzi wa nyumba. Mwanzo 2:23. Anatakiwa awe ndiye mtafutaji mkuu na kuhakikisha watu wa nyumbani kwake wanapata mahitaji yao yote. 1 Timotheo 5:8

Anatakiwa pia kuwa kiongozi wa kiroho. 1 Petro 2:9
Leo hii hatuhitaji kuhani wa kidunia kwa kuwa kila muumini ni kuhani – mshirika wa ukuhani wa kifalme wa Mungu, Na kwa kuwa mama ni kuhani wa kike, motto ni kuhani, basi baba ni kuhani mkuu hapo nyumbani. Kila asubuhi na kila jioni baba anatakiwa kuonoza familia ya makuhani na kutoa dhabihu ya sifa na maombi asubuhi nay a jioni kadiri wanafamilia wanavyokusanyika kuzunukia madhabahu ya familia.

**II. Mke ndiye moyo wa nyumba**

**A. Jukumu lake**

Ikiwa mume ndiye kichwa, basi mke ndiye moyo! Mke siyo sikio, yeye ni moyo.
Tambua jinsi alivyoumbwa. Mwanzo 2:21, 22. Mwanzo 3:16 ni kauli ya kumdhalilisha, lakini Yohana 3:16 ni msingi wa urejeshwaji wake. Hali yake iliyorejeshwa inatajwa katika Wagalatia 3:28 Moyo unadunda mara 100,000 kila siku, ukisukuma galoni 2,000 za damu iletayo uhai ikihakikisha mwili wote upo katika ulinganifu. Kwa hiyo moyo wa nyumba, yaani mke siyo tu kwamba ni mwenzi aliye sawa, bali pia ni mmoja anayeleta amani nyumbani. Kama vile tu moyo unavyodunda na kusukuma damu mwili wote, ndiyo na neema yake inavyoweza kutoa amani na umoja katika familia. Kwa hiyo yeye ni mmoja anayependezesha nyumba

### B. Uzuri wake

Siyo vito vinavyompamba, bali ni staha na adabu yake ndio uzuri wake wa kweli. 1 Petro 3:4. Kwa uzuri huu wa ndani, mke anaweza kumteka mwenzi wake asiyeamini na kumleta kwa Mwokozi wake. 1 Petro 3:1 Wito wa Mungu kwa mwanamke Mkristo: Isaya 3:16, 18-20

Wewe uliye mke, usiwe moyo mbaya! (2 Wafalme 9:30). Hebu na tuwe mioyo mizuri. Mwanzo 5:2-4

### C. Mzazi asiyekuwa na mwenzi (mzazi mmoja)

Mzazi asiyekuwa na mwenzi anakabiliwa na changamoto za pekee za kuwa kichwa wakati huo huo akiwa moyo. Lakini Mungu atawapa uwezo na hekima. (Yakobo 1:5)

## III. Upendo! Hakuna matusi!

Katika madhabahu ya ndoa hawa wawili walikuwa mmoja: 1+1 = 1. Hii ni siri au fumbo kubwa. (Waefeso 5:31, 32). Kwa kuwa mume huyu na mke wake wamepitia katika uzoefu wa siri hii ya kuwa mmoja, mwenzi mmoja hawezi kuwa na uhuru wa kumdhalilisha mwenzi wake. Hakuna mwanamume mwenye akili timamu anayeweza kujiumiza mwenyewe. Kwa hiyo hakuna mtu katika akili zake timamu anaweza kumpiga na kumdhalilisha mke wake ambaye ni sehemu yake mwenyewe. Waefeso 5:28, 29

Kwa hiyo, katika familia ya Mungu yenye furaha hakuna matusi.
Hakuna kudhalilisha na hata kuumiza mwili wa mwenzi. Hakuna kutumia maneno ya uharibifu yanayoumiza. Hakuna kudhalilisha kumhemuko kwa namna ambayo inajeruhi ile hali ya kujiamini ya mwenzi wangu. Hakuna kudhalilisha kingono ambako kunamfanya mwenzi awe duni au aharibiwe hali yake ya kijinsia.

Ikiwa matusi yatajitokeza,
Kabiliana na matusi kwa kusema kuwa, "Sitaki kuendelea kuyasikia hayo." Ikiwa maisha yanakabiliwa na hatari, ni vema kutafuta mahali salama. Ni vema pia kutafuta msaada wa kitaalam kwa yule anayetukana na yule anayetukanwa.

## IV. Kujisalimisha Kila Mmoja kwa Mwenzake

Waefeso 5:31-33 Inazuungumzia uhusiano wa mume na mke. Kaulimbiu ni ipi?
Kaulimbiu ipo katika fungu la 21. Hebu tusome hilo fungu katika Waefeso 5:21. Mke anatakiwa kumtii mume wake. Waefeso 5:22. Mume anatakiwa kumpenda mke wake kama Kristo naye alivyolipenda kanisa. Waefeso 5:25. **Swali:** Je, Kristo alijitoa kwa mahitaji ya kanisa lake? **Jibu:** Ndiyo, alijitoa hadi kutoa uhai wake kwa ajili ya kanisa lake. **Swali:** Kwa hiyo mume anatakiwa kujitoa kwa mahitaji ya mkewe? **Jibu:** Ndiyo, kujitoa hadi kutoa uhai wake kwa ajili ya mkewe. Huku ndiko kujisalimisha kwa wote wawili: Mke anajisalimisha kwa mumewe, na mume anajisalimisha kwa mkewe. Kumbuka kwamba kaulimbiu ni hii: "Jisalimishe kwa mwenzio katika kicho cha Mungu wetu." Mitume

walipokuwa wakishindana kuwa ni yupi atakuwa mkuu, Yesu alisema maneno ya kushangaza.

1. Hebu tusome katika Matayo 20:25-27
2. Kwa hiyo hakuna mkuu! Mume ni kichwa, mke ni moyo, kichwa na moyo vinafanya kazi pamoja.

**V. Pembetatu ya upendo**

Katika familia ya Mungu yenye furaha hakuna mkuu. Lakini kuna Bwana! Huyo Bwana ni Yesu! Zaburi 127:1. Hebu tuangalie katika pembetatu ya upendo pamoja na Kristo akiwa ndiye kilele. Huku ni kujisalimisha kwa hali ya juu kwa namna ambayo mume na mke wanajisalimisha kwa Kristo

**Angalia haya yafuatayo:**

Mume na mke wanapokuwa mbali na Kristo, wanakuwa mbali kutoka kwa kila mmoja. Mume na mke wanapovutwa karibu na Kristo, kwa namna hiyo hiyo wanavutwa kuwa karibu na kila mmoja. Mume na mke wanapojisalimisha kwa Kristo, wanakuwa na upendo wa kweli kwa kila mmoja wao.

**Maombi**

1. **Kila mwenzi katika ndoa kujisalimisha kwa mwenzake kwa kufuata kielelezo cha unyenyekevu wa Kristo.**
2. **Wanandoa kumweka Bwana kuwa ndiye nguzo na msingi wa kuwaungamanisha kwenye uhusiano wao**

**SOMO 2** **Novemba 3, 2019**

## MWANAMKE KUMFAHAMU MWANAMUME
## (Sehemu ya Kwanza)

### Wafilipi 4:4 "Furahini katika Bwana siku zote; tena nasema, Furahini"

**UTANGULIZI**

Jambo la ajabu ambalo yule mwenye hakima hakuweza kuelewa katika Mithali 30:18, 19. Ingawaje ni la kushangaza, tunatakiwa kuelewa msukumo wa huu mwenendo wa jinsia ya kiume kwa ile ya kike, kwa sababu haikwepeki katika mafanikio ya ndoa. Hebu tupitie na kuchunguza mambo kumi kumhusu mwanaume

**MWANAMUME WA KIDUNIA**

**I. Anaona fahari kuwa mwanaume**

Bahati mbaya jamii zingine zinamfanya mwanamke aonekane kuwa duni na kumwinua mwanaume. Jamii inamsukuma juu mwanaume; mwanamke mwenye busara hatamchana na kumshusha mumewe. Ukimwonyesha kuvutiwa naye, ataitikia kwa hisia Kila mwnamume ana vigezo vilivyo chanya. Mke mwenye busara atatambua hivyo vigezo na kuonesha kuvutiwa navyo kwa namna stahiki.

**II. Anaiangazia kazi yake**

Wakati mwanamke anaangazia au anatekwa na familia yake, mwanaume anaangazia kazi yake kwa kuwa kupitia katika kazi yake ndipo anapoweza kulisha familia yake. Hasa miaka ya mwanzo ya ajira au taaluma yake, anakuwa na msukumo wa kuweka alama yake duniani. Mwanamke mwenye busara atamtegemeza mume wake kadiri iwezekanavyo kufikia mafanikio yake. Hapa pana aya nzuri: Mithali 31:11, 12

**III. Anawasiliana kwa mambo au matendo dhahiri, siyo kwa hisia**

Kwa kawaida wanawake wanazungumza zaidi ya wanaume, wanaume wanazungumza kidogo kuliko wanawake. Wakati wanawake wanaeleza kwa hisia, wanaume wanabakika katika udhabiri wa mambo. Wanawake wanatua mizigo iliyomo mioyoni mwao kwa kushiriki na wengine, lakini wanaume wanaficha hisia zao za kweli.

**IV. Anafanya maamuzi kwa kufuata mantiki.**

Je, unakumbuka jinsi sehemu mbili za ubongo zinavyofanya kazi? Hebu tupitie:
Mwanamke anafikiria kwa namna ya tufe, mwanaume anatumia mfumo ulionyooka katika kufikiri. Mwanamke anaona kitu kwa ujumla wake ndipo atenganishe vipande; lakini mwanamume anaona sehemu zake kabla ya kuziunganisha kuwa kitu kizima.
Mke anatumia hisia katika kung'amua mambo, bali mume anatumia mantiki katika kuchambua mambo. Kwa sababu mbinu zote mbili ni za thamani, je kila mwenzi anatakiwa afanye nini? Jawabu linapatikana katika Warumi 12:10

**V. Anataka mke wake aonekane anavutia**

Mwanamume anataka aweze kusema maneno kama haya katika Wimbo Ulio Bora 4:7
Kila mwnamume ana vigezo vilivyo chanya. Mke mwenye busara atatambua hivyo vigezo na kuonesha kuvutiwa navyo kwa namna stahiki.

**VI. Anaiangazia kazi yake**

Wakati mwanamke anaangazia au anatekwa na familia yake, mwanaume anaangazia kazi yake kwa kuwa kupitia katika kazi yake ndipo anapoweza kulisha familia yake.
Hasa miaka ya mwanzo ya ajira au taaluma yake, anakuwa na msukumo wa kuweka alama yake duniani. Mwanamke mwenye busara atamtegemeza mume wake kadiri iwezekanavyo kufikia mafanikio yake. Hapa pana aya nzuri: Mithali 31:11, 12

**VII. Anawasiliana kwa mambo au matendo dhahiri, siyo kwa hisia**

Kwa kawaida wanawake wanazungumza zaidi ya wanaume, wanaume wnazungumza kidogo kuliko wanawake. Wakati wanawake wanaeleza kwa hisia, wanaume wanabakika katika udhabiri wa mambo. Wanawake wanatua mizigo iliyomo mioyoni mwao kwa kushiriki na wengine, lakini wanaume wanaficha hisia zao za kweli.

**VIII. Anafanya maamuzi kwa kufuata mantiki.**

Je, unakumbuka jinsi sehemu mbili za ubongo zinavyofanya kazi? Hebu tupitie:
Mwanamke anafikiria kwa namna ya tufe, mwanaume anatumia mfumo ulionyooka katika kufikiri. Mwanamke anaona kitu kwa ujumla wake ndipo atenganishe vipande; lakini mwanamume anaona sehemu zake kabla ya kuziunganisha kuwa kitu kizima.
Mke anatumia hisia katika kung'amua mambo, bali mume anatumia mantiki katika kuchambua mamboKwa sababu mbinu zote mbili ni za thamani, je kila mwenzi anatakiwa afanye nini? Jawabu linapatikana katika Warumi 12:10

**IX. Anataka mke wake aonekane anavutia**

Mwanamume anataka aweze kusema maneno kama haya katika Wimbo Ulio Bora 4:7
Kabla ya ndoa mwanamke alitumia muda mwingi kujiremba na kuhakikisha anaonekana wa kuvutia. Baada ya ndoa mwanamke anatakiwa kuendelea kujiremba na kuhakikisa anabakia kuvutia. Anatakiwa muda wote amshtue mume wake kwa mvuto wa mwonekano wake

**X. Mwanamume anachukia kusema, "Nahitaji msaada."**

Mwanamke mwenye busara atagundua wakati mume wake anahitaji msaada na kujitokeza kumsaidia kwa hekima. Hapa pana aya iliyotukuka: Mithali 31:26
Mazungumzo yenye busara: Usimjaze na majibu yaliyotayarishwaAnapokuwa tayari kuzungumza, msikilize. Mzungushie upendo.

## Maombi

1. **Kuombea wanawake waweze kuwafahamu wanaume kwa ajili ya kuleta furaha katika uhusiano wa ndoa na familia**

**SOMO 3** **Novemba 4, 2019**

# MWANAMKE KUMFAHAMU MWANAMUME
## (Sehemu ya Pili)

**Wafilipi 4:4 "Furahini katika Bwana siku zote; tena nasema, Furahini"**

**MWANAMUME WA KIMBINGU**

Pamoja na kwamba inafurahisha kumfahamu mwanadamu wa kidunia, inasisimua zaidi kupitia uzoefu wa mwanadamu wa kimbingu. Na huyu ni nani? Huyu ni Kristo Yesu. Hebu tupitie mambo kumi kumhusu.

### I. Kristo ni Mungu

Anaitwa "NENO" – anafanya mawazo ya Mungu yasikike. Yohana 1:13. Alikuwa na Baba tangu mwanzo kama Muumbaji mwenza. Alikuwa na ni Mungu. Yeye siye duni kwa Baba, bali ni sawa na Baba. Baba anamwita Mungu. Waebrania 1:8

### II. Alifanyika mwanadamu

Neno alifanyikwa mwili. Yohana 1:14. Hili ni fumbo lisiloweza kuelezeka! Ni kwa jinsi gani Mungu mwenye uwezo anaweza kupandikizwa kwenye tumbo la mwnamke na kuzaliwa na mwanamke ambaye ni bikira? Yeye ni Imanueli, "Mungu pamoja nasi." Alipofanyika mwili, alibakiza ile asili yake ya kimbingu na akaongezea asili ya kibinadamu. Kwa hiyo Kristo ni Mungu kamili na mwanadamu kamili. Abaitwa mwana wa Mungu na pia mwana wa Adam

### III. Akaishi maisha ambayo hayakuwa na dhambi.

Alikuwa ni fundi seremala wa Nazareti. Alikuwa ni mfanya biashara mwaminifu. Alilazimika kuuza mazao ya taaluma yake ili aweze kuishi. Alijaribiwa katika Nyanja zote kama tunavyojaribiwa. Waebrania 4:15. Lakini alimshinda Shetani. Kupitia katika uwezo wake, sisi pia tunaweza.

### IV. Kristo aliitunza Sabato

Aliumba katika Edeni na kutunza Sabato kule Palestina. Hebu tuangalie desturi na tabia yake katika Luka 4:16. Alijiita mwenyewe kama "Bwana wa Sabato." Marko 2:28. Mkristo ni mfuasi wa Kristo. Kwa sababu mimi ni Mkristo wa kweli, ni lazima niitunze Sabato ya Yesu.

### V. Yesu alibatizwa

Alikuja Yordani na kuomba abatizwe. Mathayo 3:13-16. Wakati Yohana mbatizaji alipotaka kukataa, Kristo aliye Mwokozi alisisitiza kwamba ambatize. Hakuwa na dhambi zilizotakiwa kusafishwa, lakini hata hivyo alibatizwa. Mkristo ni mfuasi wa Kristo. Kwa sababu alibatizwa, mimi pia natakiwa kubatizwa kama alivyobatizwa.

**VI. Alipitia maumivu mengi sana pale Gethsemani**

Sikiliza ombi lake la maumivu. Mathayo 26:39. Na Shetani akasimama pembeni yake akisema: "Sahau habari ya Kalvari na urudi kwenye utukufu wako!"

Katika maumivu makubwa wakati anafanya maamuzi ya mwisho, jasho lake liligeuka na kuwa matone makubwa ya damu yakitoka na kudondoka chini ardhini. Lakini ukiangalia katika karne zilizopita alikuona wewe na mimi na kusema kuwa, "Nitaenda tu hapo Kalvari." Ni upendo gani huu usiopimika!

**VII. Kristo alikufa juu ya msalaba kwa ajili yangu**

Fungu la ajabu ni hili la Luka 23:33. Rudi na kuangalia alivyochuruzika damu kwa sababu za kuchapwa mijeledi thelathini na tisa mara mbili. Pata hisia za misumari ikipenya na kuingia kwenye minofu ya mikono yake na miguu yake! Lakini zaidi ya yale maumivu ya mwili aliyopitia bado kulikuwa na maumivu ya kiakili na ya kiroho! Kristo alikuwa akipitia katika mashaka makubwa ya dhambi. Dhambi za watu wote wanaume kwa wanawake pamoja na watoto, katika nchi zote za dunia hii, katika vizazi vyote vya nyakati zote. Maumivu hayo hayaelezeki! Hebu sikiliza kilio chake cha maumivu: "Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha?" (Mathayo 27:46)

Ninapochunguza msalaba wa ajabu ambapo Mfalme wa Utukufu alifia."

Je, rafiki unampenda Yesu? Wengine wanampenda tu kwa midomo yao, lakini mioyo yao ipo mbali naye. Ikiwa nitasema kuwa, "Naam, Ninampenda Yesu" lakini "La hasha siitaki Sabato ya Yesu." Kwa kweli simpendi Yesu! Ikiwa nitasema kuwa, "Naam, ninampenda Yesu," lakini "sitaki kuongoka kwa ajili ya Kristo." Kwa kweli simpendi Yesu! Ikiwa nitasema kuw, Naam, Ninampenda Yesu," lakini "Ninakataa ubatizo wa Yesu." Kwa kweli simpendi Yesu. Ikiwa ninampenda Yesu kwa ukweli, nitaikubali Sabato ya Yesu kwa sababu Sabato ni ya Yesu. Ikiwa ninampenda Yesu kwa ukweli, nitakubali ubatizo wa Yesu kwa sababu ubatizo ni wa Yesu! Ikiwa ninampenda Yesu kwa ukweli, nitabadilika na kuongoka kwa kuwa uongofu ni wa Yesu. Njoo hapa madhabahuni usiku wa leo na kutoa maisha yako kwa Yesu.

**VIII. Alifufuka kutoka kwa wafu**

Warumi walimsulibisha Yesu. Utawala wa Rumi waliweka muhuri kwenye kaburi la Yesu. Utawala wa Rumi waliweka maaskari kulinda kaburi la Yesu. Lakini asubuhi ile ya kufufuka kwa Yesu, kwa amri ya Mungu aliye Baba, malaika aitwaye Gabrieli alipogusa ardhi, pakawa na tetemeko kuu. Ule muhuri wa utawala wa Rumi ukavunjika vipade vipande! Maaskari wa Kirumi walianguka kama wafu! Malaika wa Shetani walikimbia kwa hofu! Kristo akatoka ndani ya kaburi akiwa hai na kutamka kuwa, "Mimi ndimi huo ufufuo, na uzima. Yeye aniaminiye mimi, ajapokufa, atakuwa anaishi" Kristo ni mshindi daima!

**IX. Kristo ni Kuhani wetu Mkuu mbinguni**

Leo hii hatujitaji kuhani wa kidunia badala ya Kristo aliye Kuhani wetu Mkuu. Maandiko yanasema kuwa: Waebrania 4:14-16

**X. Yesu anakuja tena!**

Ahadi yake yenye thamani: Yohana 14:1-3. Mandhari, ni utukufu mtupu! 1 Wathesalonike 4:16. Atarudi akiandamana na mabilioni ya malaika wakiangaza mbingu

Kutakuwa na ufufuo, muunganiko, na kupaa**.** Mungu ataumba upya dunia yetu hii na kuifanya paradise yenye Amani. Tutakuwa familia ya Mungu yenye furaha milele na milele

## Maombi

1. **Mungu atusaidie kuitikia ukombozi aliotupatia katika Kristo kwa kuyasalimisha maisha kwake kama Bwana na Mwokozi wetu**
2. **Shauku ya kuishi maisha matakatifu kwa neema ya Mungu**

**SOMO 4** **Novemba 5, 2019**

# MWANAMUME KUMFAHAMU MWANAMKE
## (Sehemu ya Kwanza)

**Wafilipi 4:4 "Furahini katika Bwana siku zote; tena nasema, Furahini"**

**UTANGULIZI**

Wanaume na wanawake wanatofautiana kibailojia, kimhemuko, na hata kimwenendo. Ikiwa wenzi wawili wanataka kuishi pamoja kwa furaha, mwanamume anatakiwa kuelewa njia za mwanamke. Hebu tutazame mambo kumi ambayo kila mwanamume anatakiwa kufahamu kuhusu wanawake.

**SEHEMU YA KWANZA: MKE**

**II. Mwanamke**

Katika jamii ambayo wanaume wana amri juu ya wanawake, mwanamke mara nyingi anafanywa kuwa duni. Hali kama hiyo inamfanya mwanamke kupoteza hali yake ya kujiamini. Mume mwenye busara atamthibitisha mke wake akimwezesha kujiamini.
Hapa pana aya muhimu. Mithali 16:24

Mwenzi anayejali atamtambua mwenzi wake na kuonesha wazi wazi kutambua kile chema mwanamke anachofanya. Kwa mfano, chakula kizuri alichopika, namna alivyopangilia vitu hapo nyumbani, uaminifu wake, mambo mengine yanayohitaji kusifiwa au kupongezwa. Kutambua na kupongeza kunaweza kuoneshwa kwa: Kumbuka siku ya kuzaliwa, kumbukumbu za shereha mbali mbali na siku maalum unazofahamu. Zawadi na vitu vidogo vidogo vya kushtukiza.

**II. Anafurahia kusaidiwa katika shughuli za nyumbani.**

Hebu pitia aya hii katika Wagalatia 6:2. Mkono wa mwanamume unatakiwa kuinuliwa siyo tu wakati wa kumkumbatia mkewe, bali pita katika kumsaidia. Wanawake wa nyumbani wanachoka na huwa wanafurahia kusaidiwa. Wanawake walioajiriwa wanachoka pia na wanahitaji kusaidiwa. Wenzi wenye mapato pande mbili (mwanamume na mwanamke) wanatakiwa kusaidiana kazi za nyumbani. Ikiwa wote wanafanya kazi nje ya nyumbani, wote wanatakiwa kufanya kazi kwa pamoja nyumbani pia.

**III. Anaonesha hisia zake na anahitaji sikio linalosikia. (asikilizwe)**

Wanaume wanajielekeza katika ukweli wa mambo, lakini wanawake wanaonyesha tu hisia zao. Mwanamume mwenye busara atatenga muda kumsikiliza mkewe kwa uvumilivu.
"Basi kila *mume* na awe mwepesi wa kusikia" (Yakobo 1:19)

**IV. Mwanamke anabadilika kirahisi, hisia na hali mbali mbali zinabadilika badilika.**

Hii ni kwa sababu ya kemikali za mwili. Damu ya mwanamke ndani ya mishipa ina oksijeni iliyopungua kwenye chembe chembe nyekundu za damu kwa asilimia 20 kuliko kwa mwanamume. Kisha kuna mzunguko wa mwanamke wa hedhi. Huu mzunguko wake wa kila mwezi unasababisha mabadiliko ambayo yanasababisha fadhaa inayoathiri mwenendo wa mhemuko.

**V. Mwanamke ni mdhaifu, lakini ni imara. Yeye ana:**

Anasikia kwa makini, anaona vyema usiku kuliko mwanamume na ana uwezo wa kunusa kuliko mwanamume. Ana mfumo imara wa kinga ya mwili. Uwezo mkubwa wa kuzuia magonjwa ya moyo kwa kipindi ambacho bado ana uwezo wa kupata uja uzito. Ana utepe unaounganisha ubongo ulio imara hivyo kuweza kuhimili kiharusi na kupona haraka. Anaishi maisha marefu ukilinganisha na mwanamume kwa takribani miaka minane.

**VI. Anayo karama ya jicho la tatu – anafikia hitimisho bila kushawishiwa.**

Sehemu mbili za ubongo wa mwanamke zinafanya kazi kwa namna tofauti. Ubongo wa kushoto unachakata taarifa kwa msitari, lakini ubongo wa kulia unachakata taarifa kwa mduara. Ubongo wa kushoto unatumia sehemu katika kuunda kitu kizima lakini ubongo wa kulia unaona vitu kwa ukamilifu wake kabla ya kuangalia sehemu zake.

Ubongo wa kushoto unatatua matatizo kwa mantiki lakini ubongo wa kulia unatatua matatizo kwa kujaribu. Ubongo wa kushoto unatumia uchanganuzi lakini ubongo wa kulia unatumia usanisi. Wanawake wanatumia ubongo wa kushoto zaidi kuliko wanaume. Kwa sababu hiyo ni wepesi wa kung'amua kitu kuliko mwanamume. Kwa kutambua karama hii, mwanamume mwenye busara atamsikiliza mke wake. Ushauri wa Kristo ni huu katika Marko 4:23

**VII. Mwanamke anaamshwa kwa kile anachohisi.**

Wakati mwanamume anaamshwa kwa kuona, mwanamke anaamshwa kwa namna anavyohisi. Soma fungu la Wimbo Ulio Bora 2:6

Mwanamume mwenye busara anatenga muda wa kutosha kwa vitendo muhimu vya kumwamsha mke wake kwa matayarisho ya ule ukaribu wa tendo la ndoa akitambua kuwa ni pale tu wenzi wote wawili wanapokuwa tayari ndipo watakapofikia upeo wa juu wa kuridhishana.

**VIII. Mwanamke anafurahia namna mbali mbali za kuonesha upendo**

Kuna namna tatu za kuonesha upendo: Kawaida tu – kwa kumshika mkono tu

Kwa ukaribu wa pekee – kukumbatia na kubusu. Utimilifu au kuonesha kwa tendo la ndoa.

Mwanamume anaanza kutoka 1 kwenda 2 hadi 3

**Lakini mwanamke:** Wakati mwingine mwanamke anatua katika namba moja. Wakati mwingine anatua katika namna mbili. Wakati mwingine anaendelea hadi namba tatu. Kwa hiyo ushauri wa Mungu ni upi? Warumi 12:10

**IX. Mwanamke anahitaji yai jipya katika kiota chake kilicho kitupu.**

Nyakati tofauti kwa mambo tofauti. Mhubiri 3:1. Katika hatua mbali mbali za maisha mwanamke anarekebisha mtazamo wake. Wakati wenzi ndiyo tu wameoana, mtazamo wa mwanamke ni mwenzi wake na hitaji la ukaribu wa faragha naye. Anapoana kupata watoto, mtazamo wake unahamia kwa watoto na hitaji lake ni katika familia. Watoto wanapokuwa wamekua na kuondoka nyumbani kiota kunabakia kitupu, mtazamo wake unamgeukia yeye mwenyewe na hitaji lake wakati huo ni kutafuta kujitambua na kujiridhisha.

Kwa hiyo watoto wake wanapokua na kuondoka nyumbani, anaingia katika hatua ya kutaka mayai mengine mapya, shughuli mpya ili kujiridhisha. Mwanamume mwenye busara atakuwa mwangalifu kutamua mabadiliko ya mahitaji ya mke wake na kumwezesha katika mabadiliko hayo. Hebu tutulie hapa kidogo nakumgeukia mwanamke wa kiroho. Baadaye tutarudi kuona vipengele kumi vya mwanamke wa kidunia.

## Maombi

1. **Mwanaume amfahamu mwanamke na mahitaji yake ili wadumishe uhusiano wa ndoa**
2. **Wamaume kujua namna ya kuishi na mwanamke kwa akili**

**SOMO 5** **Novemba 6, 2019**

## MWANAMUME KUMFAHAMU MWANAMKE
## (Sehemu ya Pili)

### Wafilipi 4:4 "Furahini katika Bwana siku zote; tena nasema, Furahini"

**KANISA**

Katika Maandiko, mwanamke anatumiwa kwa ishara ya kanisa la Kristo. Waefeso 5:25, 32. Kwa namna tunavyoendelea kujifunza mambu kumi yanayomhusu mwanamke wa duniani, ambaye ni mke, hebu tuangalie mambo kumi yaliyo ya kweli kuhusu mwanamke wa kiroho, yaani kanisa. Katika Ufunuo 14 tunaambiwa kuhusu mafundisho ya kanisa la Kristo, lakini. Katika Ufunuo 12 tunaambiwa kuhusu pambano la kanisa la Kristo

**A. Mafundisho**

Kanisa la Kristo linahubiri Injili ya milele. Ufunuo 14:6
Injili ni habari njema za wokovu. Ni ya milele, haibadiliki. Ni la kimataifa – linaenda kwa kila taifa. Linahubiri katika kila nchi, kila taifa, na kila lugha. Linatangaza kwamba saa ya hukumuu ya Mungu imefika. Ufunuo 14:17. Saa ya hukumu ya Mungu Ilianza mwaka 1844
Kanisa la Mungu linawaita watu waabudu katika Sabato ya kweli. Huu ni wito wa kumwabudu Mungu wa uumbaji. Hii ni nukuu ya moja kwa moja kutoka katika amri ya nne. Kwa hiyo, kanisa la Kristo linatangaza ibada ya Sabato.

Linapaza sauti kutoka katika Babeli. Ufunuo 14:8. Babeli maana yake ni machafuko (Kumbuka ule mnara wa Babeli?) Babeli inaashiria machafuko yatokanayo na mchanganyiko wa ukweli na uongo. Linawaonya watu dhidi ya mnyama, sanamu na alama yake. Hebu tazama aya hii ya ajabu. Ufunuo 14:9-11. Mnyama huyu ni mamlaka ya Rumi. Sanamu ya mnyama ni satellite ya Rumi. Alama ya mnyama ni ibada ya Jumapili iliyoamuriwa na Rumi. Alama katika vipaji vya nyuso na katika mkono maana yake ni fikra na matendo. Ghadhabu ya Mungu ni mapigo saba ya mwisho na hatimaye moto wa kuzimu.
Linatunza amri zote kumi za Mungu. Ufunuo 14:12. Kanisa hilo linatunza amri kumi za Mungu – siyo ili lipate kuokolewa bali kwa sababu limeshaokolewa. Linaokolewa kwa neema - kwa Imani ya Yesu. Ufunuo 14:12. Tunaokolewa kwa neema. (Waefeso 2:8)
Kanisa la Kristo linapitia katika mateso. Katika Ufunuo 12 tunasoma pambano la kanisa likionekana katika historia yote. Kanisa la Kristo lilistahimili mateso.

**B. Pambano**

Vita pale Bethlehemu. Ufunuo 12:1-5. Huyu mwanamke aliyevikwa utukufu ni kanisa la kweli la Kristo. Mwanamke aliye na utungu akikaribia kuzaa, ni wakati wa kuzaliwa kwa Yesu. Joka kubwa jekundu linawakilisha mamlaka ya Rumi

Joka alijaribu kumwangamiza mtoto inaashiria mamlaka ya Rumi ilivyojaribu kumuua mtoto Yesu. Mtoto mwanamume anayenyakuliwa hata mbinguni kwa Mungu anawakilisha kupaa kwa Kristo kwa ushindi.

**Kizuizini kule nyikani:** Ndipo kanisa likakimbilia nyikani. Ufunuo 12:6. Kwa kuwa siku moja katika uabii wa Biblia inawakilisha mwaka mmoja (Ezekiel 4:6) kanisa lilikuwa kizuizini kwa miaka 1260. Kipindi hiki cha miaka 1260 kilikuwa kati ya mwaka 538 hadi 1798 Baada ya Kristo. Sehemu kubwa ya kipindi hiki iliitwa "Zama za Giza". Kulikuwa na giza la kiroho kwa sababu Biblia zilifungiwa katika majumba ya watawa na watu wa kawaida hawakuruhusiwa kuzisoma. Ukweli ulikuwa nyikani! Udanganyifu ulikaa katika kiti cha enzi. Kwa hiyo mafundisho ya uongo yaliongezeka. Baadhi yake ni haya hapa: Ibada ya Jumapili. Ubatizo wa watoto wachanga. Kuwaenzi watakatifu na kuwapatia hadhi. Tohorani. Kuungama kwa viongozi wa kanisa (kwa maaskofu). Kujitesa ili kusafisha dhambi. Kuwaombea wafu.

Pambano la Wanamatengenezo. Habari njema ni kwamba ingawaje ukweli ulihamishiwa kizuizini, bado ulilindwa.

Kanisa hilo liliendelea kuhubiri kutoka nyikani na muda si mrefu nuru ya ukweli ilianza kuangaza kwenye giza la uongo! Mungu aliinua watu na makundi mbalimbali ili kutangaza kweli mbali mbali. Katika karne ya 16 aliwainua Waluteri ambao walieneza ukweli wa neema ya Yesu. Tumshukuru Mungu kwa kazi nzuri ya Waluteri. Katika karne ya 17 aliwainua Wabatisi wakifundisha ukweli wa ubatizo wa Yesu. Tumshukuru Mungu kwa kazi nzuri ya Wabaptisi. Katika karne ya 18 Mungu aliwainua Wesley na Wamethodi waliotangaza ukweli kuhusu kazi ya Yesu. Tumshukuru Munguu kwa kazi nzuri ya Wamethodi. Katika karne ya 19 Mungu aliwainua Waadventista wa Sabato kutangaza habari ya Sabato ya Yesu na kuja mara ya pili ya Yesu. Hawa walikusanya kweli zote zilizogunduliwa na kuitangazia dunia injili ya milele.

**Wito wa Yesu:** Leo hii Kristo anao watu wake waaminifu katika dini zote zilizoki duniani. Dini za Wakristo na wasio Wakristo, Mungu anao watu wake waaminifu. Hapa pana aya ya ajabu katika Yohana 10:16**.** Je, wewe ni kondoo wa Kristo? Je, unaisikia sauti yake? Usiku wa leo, Kristo anawaita watu wake waaminifu kutoka kila mahali waje katika kanisa lake la Masalia. Hebu pitia katika aya hii yenye nguvu: Ufunuo 18:4**.** "Watu wangu." Je, wewe ni miongoni mwa watu wake? Je, unasikia sauti yake ikiita? Je, mwitikio wako utakuwaje?

Swali: Je, ninakuwaje sehemu ya Masalia ya Kristo? Jawabu: Kwa kubatizwa. (Wakorintho 12:13)

## Maombi: Kutambua wakati tunaoishi na kujiandaa kwa kuja kwa kristo

**SOMO 6** **Novemba 7, 2019**

## CHANGAMOTO NA BARAKA ZA MAKAPERA/WASEJA

### (Sehemu ya Kwanza)

### Wafilipi 4:4 “Furahini katika Bwana siku zote; tena nasema, Furahini”

**UTANGULIZI**

**Kisa:** Hapo zamani za kale, palikuwapo na binti ambaye alikuwa hajaolewa. Yeye alitoa maagizo ya maziko yake, na moja ya agizo ilikuwa kwamba wote watakaobeba jeneza lake wawe ni wanawake! Sababu yake ilikuwa ni nini? Kwa sababu vijana wa kiume walikuwa wameshindwa kufanya naye urafiki wakati wa uhai wake, basi wasije wakaruhusiwa kubeba jeneza lake katika maziko yake. Baadhi ya watu hapa hawajaoa wala kuolewa, ni wachungu na wanyonge, lakini kuna wengine hawajaoa wala kuolewa lakini wanavutia. Ni nini kinaleta tofauti?

**NGAZI YA KIJAMII**

**A. AINA MBALIMBALI ZA MAKAPERA/WASEJA**

Wale ambao bado wanatafuta. Hawa wanatazamia kubadilisha hali yao hapo watakapompata yule aliye sahihi. Hapa pana ushauri kwa hao waliopo katika kundi hili:
Shiriki katika shughuli mbali mbali za kijamii ili kukutana na watu wengi na kujichanganya. Dumisha hali yako ya kuvutia kimavazi hata mwonekano. Shinda aibu na hofu. Boresha mawasiliano na stadi za mahushiano. Tambua kwamba hautaweza kupata mtu aliye mkamilifu kwa sababu wewe mwenyewe siyo mkamilifu. Omba uongozi wa Mungu. Yule Mungu wa Isaka anaweza kuwa Mungu wako. (Mwanzo 24)

Wale walioamua kuwa makapera au waseja kwa hiari yao wenyewe. Watu kama hao, wamehiari kubakia hivyo (kutooa/kutoolewa) badala ya kufungwa katika ndoa. Waliotengana au waliotalikiana. Hawa ni wale ambao wamepitia mshutuko wa machungu ya mahusiano yaliyovunjika. Wagane/wajane. Hawa wamepitia uzoefu wa kupotelewa na wenzi wao kwa ule mkono katili wa mauti. Katika hali yoyote itakayosababisa mtu kujikuta bila mwenzi, hapa kuna hatua saba za kubakia mzuri na unayevutia.

**B. HATUA SABA KIJAMII**

Ishi kwa kutazamia mema.
Katika kitabu cha Mithali 17:22 kuna sababu nzuri ya kuishi kwa kutazamia mema. Wale walio makapera/waseja wanakutana na changamoto na hivyo wanatakiwa kudumisha mtazamo chanya katika maisha, kwani kusihi kwa kutazamia mema ni uchaguzi binafsi.

Pale uzoefu wa zamani ulio hasi unapokunyemelea na kukufanya utazamie mabaya, ni vyema kufuata ushauri uliopo katika kitabu cha Wafilipi 3:13

**Tambua hadhi na heshima ya kuwa kapera au mseja**
Soma fungu hili lenye nguvu: 1 Wakorintho 7:7. Mtume Paulo alikuwa kapera (yaani hakuwahi kuoa) wakati alipoandika waraka kwa Wakorintho. Tambua kwamba aliita ile hali ya kuwa kapera au mseja kuwa moja ya "karama." Kwa hiyo kama vile ndoa ilivyo karama, useja au ukapera pia ni karama. Kwa sababu hiyo, hali ya kuwa kapera/mseja inatakiwa kuchukuliwa kwa hadhi na heshima sawa na hali ya kuwa katika ndoa. Chanzo halisi cha furaha siyo kuwa katika ndoa, bali ni ile hali ya kuwa karibu sana na Mungu wako. Zaburi 16:11

**Hesabu mibaraka yangu**
Maisha ni kama mti wa maua ya waridi ambao una maua mazuri lakini pia una miba. Ndoa ina maua yake na miiba yake, na useja au ukapera pia una maua yake na miba yake.

Baadhi ya miba ya ukapera au useja ni: Upweke, Ukosefu wa starehe ya ngono, Jamii kutokupokea vizuri hali ya kutokuoa/kutokuolewa. Baadhi ya maua ya ukapera au useja ni: Uhuru wa kumiliki na kutawala muda wako utakavyo, Uhuru wa kwenda popote utakapo bila kumuuliza mtu, Kutawala fedha zako jinsi utakavyo. Uhuru wa kutimiza malengo binafsi ya ajira

Imarisha hali ya kujiamini.
Iwe nimeoa/olewa au sijaoa/olewa, mimi ni wa thamani! Hapa kuna aya ya ajabu kwangu: Isaya 43:4. Ndoa haiongezei thamani yangu. Ukapera au useja haupunguzi staha yangu. Iwe nimeoa/olewa au sijaoa/olewa, mimi ni wa thamani kwa Mungu kama nilivyo wa thamani katika jamii.

Baadhi ya waseja/makapera waliobariki dunia ni kama:

i. Florence Nighingale – Mwanzilisi wa fani ya uuguzi
ii. Sir Isaac Newton – Gwiji wa mahesabu na fizikia
iii. 9zzEvangeline Booth – Jenerali wa kike wa Jeshi la Wokovu
iv. Ludwig Van Beethoven – Mwanamziki Mjerumani na mtunzi wa nyimbo
v. Marion Anderson – Mmarekani mwanamke mwimbaji mashuhuri wa sauti ya kiume
vi. Ikiwezekana unaweza kuongezea watu wengine mashuhuri unaowafahamu katika mazingira yako.

Na katika Biblia pia tunao waseja/makapera waliokuwa mashuhuri:

i. Mtume Paulo – Mwanatheolojia Mkristo aliyekuwa mashuhuri sana

ii. Dorcas – Mfanyakazi wa kijamii mashuhuri katika historia
iii. Yesu Kristo, Bwana na Mwokozi wetu.

Kuwa mtu wa kujitegemea kiuchumi (kifedha)

Hapa kuna usharui wenye hekima: 1 Wathesalonike 4:11, 12

Ikiwa mimi ni tegemezi kiuchumi basi ninakuwa dhaifu. Ili niweze kujitegemea, ninahitaji stadi kielimu au kiteknolojia, zitakazoniwezesha kuishi kwa mafanikio. Kwa hiyo ni lazima nipate elimu kamilifu, Au niwe na stadi fulani muhimu, Ikiwa sijaoa/olewa lakini nina watoto au mtoto, na ninataka kumfuata Yesu, ninatakiwa nifanye haya: Kuoa/kuolewa kama kuna uwezekano na pia kama kuna haja. Ikiwa hakuna uwezekano wa kuoa/kuolewa, basi ni vyea kusitisha uhusiano huo. Kufanya kazi ili kujitegemeza mwenyewe pamoja na mtoto au watoto nilio nao. Kufanya sehemu yangu na kumtumaini Mungu kwamba atawezesha fmilia yangu. (Mathayo 6:33)

Tawala mihemko ya kingono kwa hekima

Kwanza, kwa kujizuia. Yakobo 4:7 Weka katika utendaji uwiano wa mafanikio ya kiroho

i. Nia ya kibinadamu + Uwezo wa Kimbingu = Ushindi wa kiroho.
ii. Kwa namna nyingine: kile ninachochagua + Maombi yangu = Ninaweza.

Ninaweza kutumia mbinu ya kuhafifisha na kubadili mwelekeo

i. Kuhafifisha ni kuelekeza nguvu zako katika mwelekeo tofauti kuliko ule uliokuwa umezoea.
ii. Kubadili mwelekeo wa nguvu zako na kuzielekeza katika shughuli ambazo ni chanya kunaweza kukuletea kuridhika kimhemuko na kimwili.
iii. Bila shaka huu ndio ulikuwa ni uzoefu wa Dorka. Wakati alipokuwa akiwabariki wengine, alijikuta akipata namna fulani ya kuridhika kimwili na kimhemuko

a. Maandiko yanahimiza kubadili mwelekeo. Warumi 12:21

Mfanye Kristo awe ndiye mwenzi wa karibu muda wote

**SOMO 7** **Novemba 8, 2019**

## CHANGAMOTO NA BARAKA ZA MAKAPERA/WASEJA
## (Sehemu ya Pili)

### Wafilipi 4:4 “Furahini katika Bwana siku zote; tena nasema, Furahini”

**NGAZI YA KIROHO**

**A. KISA CHA MARIAMU.**

Hapo zamani za kale palikuwapo na binti aliyeitwa Mariamu. Alikuwa hajaolewa, mzuri na wa kuvutia. Aliishi katika kijiji kidogo cha Bethania pamoja na dada yake aliyeitwa Martha na kaka yake kwa jina la Lazaro. Bahati mbaya mtu mmoja aitwaye Simoni aliyekuwa Farisayo alimwingiza Mariamu katika uzinzi. Mariamu akahamia Magdala na kufahamika kama Mariamu Magdalena. Akiwa amezama katika uovu huo aligeuka kituko ana kutumiwa kama mfano kwa ukahaba. Baada ya wakati Shetani alimfanya mtumwa. Mawazo yake na mwili wake ukawa ni makao ya mapepo. Wakati huu alikuwa hajaolewa, lakini akiwa na uchungu na duni. Lakini siku moja Yesu alitembelea Magdala na vita ya Mariamu ikaanza! Yale mapepo yaliyofanya makao kwake yakaanza kutoka moja baada ya jingine, na Kristo akapata ushindi. Hebu tusome kuhusu habari hii katika Luka 8:2. Mariamu akapiga hatua saba kutoka katika kushindwa hadi katika mafanikio, kutoka katika hali ya uchungu na kuwa duni hadi kuwa na mzuri na wa kuvutia. Hatua saba za kiroho. Ikiwa yeye alichukua hatua hizo, sisi pia tunaweza kuzichukua

**HATUA SABA ZA KIROHO**

**Kutoa maisha yangu kwa Yesu**

Hapa kuna aya ya ajabu: 2 Wakorintho 5:17. Mara tu Mariamu alipotoa maisha yake kwa Kristo, alibadilika akawa Mariamu mpya. Akarudi na kuwa mseja tena, mzuri na wa kuvutia.

Alikuwa mtu mpya, kutoka katika kkuwa mwenye dhambi, hadi kuwa muumini mpya. Alimtumikia Bwana mpya, badala ya Shetani alianza kumtumikia Yesu. Alipata kazi mpya kutoka katika ukahaba hadi kwenye kuwa mwanafunzi wa Yesu. Kile Yesu alichofanya kwa ajili ya Mariamu, anaweza kukifanya kwako na kwangu pia.

**Kumimina upendo wangu kwa Yesu**

Sasa tazama kile alichofanya katika Luka 7:38. Kwa nini alifanya hivyo? Kwa sababu moyo wake ulikuwa umejawa na upendo. Akiwa amesimama pale, alikumbuka kuwa: Ndipo mwili wake wote ulitetemeka kwa mhemuko mtakatifu! Asingeweza kuzuia machozi yake. Kwa unyenyekevu alipangusa vumbi kutoka katika miguu ya yesu kwa machozi yake, akaikausha na nywele zake, na kuibusu, akimwaga manukato katika mwili wake. Rafiki, jambo kama hili limeshawahi kutikea kwako? Je, upendo wa Yesu umewahi

kukusisimua tena na tena? Hebu upendo wake na ububujike kupitia kwako usiku wa leo. Ndipo nafsi yako itaweza kuimba wimbo wa upendo kwa Yesu, "Yesu Nakupenda U Mali Yangu."

**Kutoa kafara yangu kwa Yesu**
Je, Mariamu alitumia marashi gani? Hebu tuone katika Marko 14:3. Marashi yale yalikuwa ya gharama sana! Marashi hayo yaligharimu malipo ya mwaka mzima ya mfanyakazi wa kawaida. Malipo ya siku wa mfanya kazi wa kawaida yalikuwa ni dinari moja au sarafu ya kirumi (Mathayo 20:2). Kwa hiyo zawai hii iliwakilisha mshahara wa mwaka mzima. Hiyo ilikuwa ni kafara kubwa sana!

Leo hii, Mungu anakuuliza wewe na mimi kwa kutoa maisha yetu kwake kama kafara iliyo hai. Warumi 2:1. Hii ndiyo maana ya ubatizo – ni kafara iliyo ya kufurahisha. Je, unampenda Yesu kiasi cha kumtolea hiyo kafara?

**Kusimama upande wa Yesu**
Ni wakati wa Ijumaa Kuu! Yesu ananing'inia akiwa amesulubiwa pale Kalvari. Yuda Iskariote alikuwa wapi wakati huo? Alikuwa amejinyonga. Petro je, alikuwa wapi? Alikuwa amemkana Bwana wake. Filipo na andrea, Yakobo na Matayo je, walikuwa wapi? Walikuwa wamekimbia kwa hofu.

Mariamu alikuwa wapi? Hebu soma jibu lenye nguvu katika Yohana 19:25. Alikuwa amesimama kwa ujasiri pale Kalvari. Alionesha msimamo wake hadharani mbele ya wale waliokuwa wakimbeza na wauaji! Bila woga alidhihirisha kwamba yeye alikuwa ni wa Kristo aliyesulubiwa. Ndugu yangu, simama upande wa Kristo usiku wa leo! Dada yangu, simama upande wa Kristo usiku wa leo.

**Kushika Sabato ya Yesu**
Ndipo walipomweka Mwokozi kaburini. Siku ile iliyokuwa ni Sabato ya Edeni, Kristo alipumzika kutoka katika kazi yake ya uumbaji. Katika siku hii ya Sabato ya Kalvari, alipumzika kutoka katika kazi yake ya ukombozi. Wakati Kristo akipumzika kaburini, Mariamu pia aliadhimisha na kupumzika Sabato. Hebu pitia ayah iliyo muhimu: Luka 23:55, 56. Sabato inayokuja itakuwa ni Sabato ya pekee ya kusherehekea! Yesu atakuwa hapa. Malaika pia watakuwa hapa! Ni lazima wewe pia uwe hapa!

**Sikia sauti ya Yesu akikuita kwa jina lako**
Jumapili asubuhi ikawadia. Mariamu anaelekea bustanini. Lakini mwili wa Yesu haupo kaburini! Ndipo anapomwona "mtunza bustani" na anajaribu kumsemesha. Hebu sikiliza mazungumzo yaliyonukuliwa katika Yohana 20:15, 16. Mariamu akasema: "Bwana, ikiwa umemchukua wewe, uniambie ulipomweka, nami nitamwondoa." "Yesu akamwambia, Mariamu." "Yeye akageuka, akamwambia kwa Kiebrania, Raboni! (Yaani, Mwalimu

wangu).” Kumbe alikuwa ni Yesu! Sikiliza! Je, unamsikia? Kwa namna aliyomwita Mariamu, vivyo hivyo anakuita wewe kwa jina lako! Je, jibu lako litakuwaje?

**Kuheshimiwa na Yesu**
Ndipo Yesu akatamka kauli ya kushtua. Hebu tuisome katika Yohana 20:17
Hili ni jambo la ajabu! Kabla Yesu hajapaa kwenda Baba yake wa mbinguni, alisubiri ili amwone Mariamu Magdalena. Ni wazo la ajabu hili. Kabla Baba hajamwamkia, Mariamu alikutana naye! Kabla malaika hawajamsujudia, Mariamu alimsujudia!
Mwanadamu wa kwanza kumwona Bwana aliyefufuka alikuwa ni mwanamke wala siyo mwanaume. Na huyo mwanamke hakuwa ameolewa, alikuwa ni mseja! Ninapojitokeza kumfuata Yesu, ataniheshimu hata kama mimi ni wa jinsia ya kike au ya kiume, niwe nimeoa/olewa au sijaoa/olewa. Ataniheshimu kwa kunifanikisha katika maisha haya. (Torati 28:13). Kristo atakapokuja katika utukufu, ataniheshimu kwa kunipatia furaha ya uzima wa milele (Ufunuo 2:10)

## UAMUZI

**Wimbo wa upendo:** Kwa hiyo wimbo wetu usiku wa leo ni wimbo wa kumpenda Yesu, “Yesu Nakupenda, U mali Yangu.” Basi tusimame na kuimba.

**Vijana:** Usiku wa leo wito wa kwanza wa Mungu ni kwa ajili yenu, ninyi mlio vijana wa kiume na wa kike. Mwovu ana mpango kwa ajili ya maisha yenu ili kuyafanya yawe na uchungu na kuwafanya kuwa duni, lakini Mungu ana mpango m-badala, kufanya maisha yenu kuwa mazuri na ya kuvutia. Chagua upande wa Mungu usiku wa leo. Mpatie Yesu Kristo maisha yako. Sogea mbele hapa sasa.

**Uponyaji:** Usiku wa leo Mungu yuko tayari kukupatia wokovu, uwe mzee au kijana, umeoa/olewa au haujaoa/olewa, uwe jinsia ya kiume au ya kike, kama vile alivyomponya Mariamu. Atawakemea na kuwafukuza mapepo ikiwa utamwomba. Je, unataka ayaondoe mapepo ya anasa za dunia hii? Tembea uje mbele hapa kwenye madhabahu. Je ungependa aondoe na kutupilia mbali mapepo ya tumbaku, pombe, madawa ya kulevya na mahangaiko mengine? Sogea kwenye madhabahu hapa. Je, ungependa akemee na kutupilia mbali mapepo ya uzinzi na uasherati? Mapepo ya unyanyasaji wa kijinsia? Soge mbele hapa kwenye madhabahu muda huu huu wala usichelewe.

1. **Mrindimo wa upendo.** Fungua kijaluba chako cha marashi na kuipaka miguu ya Yesu. Hebu upendo wake ukusababishe kurindima na kutetemeka kwa mhemuko mtakatifu. Hebu upendo wa Yesu ububujike katika roho yako usiku wa leo. Je unausikia? Basi sogea mbele hapa kwenye madhabahu sasa hivi.

2. **Kafara.** Mariamu alitoa kafara akiba yake aliyokuwa ametunza maisha yake yote kwa namna alivyotoa kila kitu kwa Yesu. Je, usiku wa leo Mungu anataka

utoe na kumpa nini? Ni nini hicho anachokutaka utoe kafara? Chochote kile anachotaka, ungesogea tu mbele katika madhabahu na kujitoa kikamilifu?

3. **Inuka usimame.** Watu wanageukia upande wa Yesu. Simama juu, njoo hapa madhabahuni. Kina mama, dada wazuri, simama upande wa Yesu. Ikubali Sabato yake, kubali ubatizo wa maji mengi, simama upande wa Yesu.

4. **Jina.** Je unamsikia akikuita kwa jina lako? Kijana, Mungu ana mpango kwa ajili ya maisha yako. Binti, Mungu anao mpango kwa ajili yako. Njoo madhabahuni na ujiunge katika mpango wa Mungu sasa hivi.

5. **Heshima.** Mariamu aliheshimiwa. Mwanadamu wa kwanza kumwona Bwana amefufuka alikuwa ni mseja, mzuri na anayependeza. Huyu ndiye aliyebahatika na kuheshimika. Mungu atakuheshimu katika maisha haya ikiwa utakuja madhabahuni. Ndipo atakapokuheshimu kwa kukupatia uzima wa milele. Je utasoge na kuja ili upate mibaraka sasa? Haya njoo.

**Maombi: Washiriki wataje mambo ya kuombea**

**SOMO 8** **Novemba 9, 2019**

# HATUA ZA MWANA MPOTEVU

## Wafilipi 4:4 "Furahini katika Bwana siku zote; tena nasema, Furahini"

**UTANGULIZI**

**Kisa:** Tania alipaza sauti yake na kusema, "Mimi siyo mtoto tena!" akaendelela kusema, "Mimi ni mtu mzima, na natakiwa kuchukuliwa kama mtu mzima!" Mzazi wake aliitikia kwa kusema, "Wewe bado ni mtoto." Akatulia kidogo kisha akaendelea kuwa, "Na wakati wewe ukiwa bado chini ya dari yangu, utafanya kama ninavyosema bila kuuliza maswali!" Kwa hiyo, kwa majibizano hayo ni nani alikuwa sahihi? Miaka ya ujana ni changamoto kwa sababu vijana wanapopevuka, wanajiona kuwa siyo watoto tena, lakini wakati huo huo bado hawajawa watu wazima.

## FAMILIA YA KIROHO

Yesu alieleza kisa cha kijana mkorofi mwenye uasi na mzazi wake aliyekuwa mvumilivu**.** Alitoa kisa hiki kwa sababu mbili:

- Kuonesha jinsi Mungu ambaye ni Baba yangu anavyonipenda bila masharti.
- Kunigusa mimi kama mzazi kwa jinsi ninavyotakiwa kumpenda mtoto wangu bila masharti.

Kisa hiki kinaanzia katika Luka 15:11, 12. Kijana huyu alikuwa na matatizo. Nyumbani palionekana kama gereza, na baba yake kama msimamizi wa gereza. Sheria nyingi zisizo na maana! Makatazo mengi! Alitaka uhuru. Alitaka kufanya kila alichoona bora kufanya.

Sisi pia huwa tunamwambia Mungu hivyo hivyo.
Sheria nyingi zisizo na maana! Makatazo mengi! Ninataka kuwa huru! Huru kufanya jinsi ninavyotaka, kula na kunywa kile ninachotaka, kuvaa kama ninavyotaka, kuishi kama ninavyotaka.

### A. HATUA TANO ZA KUPOTEA

**I. Uasi: Luka 15:12**

Huyu alikuwa kijana mfedhuli. Alipaza sauti akasema, "Baba, nipe sehemu ya mali inayoniangukia!" Alikuwa na roho ya uasi, akimpinga baba yake aliyempenda wazi wazi na kumfanya mama yake asikome kulia kwa maumivu.

**II. Nchi ya mbali: Luka 15:13**

Alikata tiketi kwenda mbali kiasi ambacho iliwezekana. Mbali kutoka kwa ulinzi wa mama yake, mbalikutoka kwa upendo wa baba yake. Baadhi ya watoto wa Mungu waliopo hapa usiku wa leo wamekimbia kwenda nchi za mbali. Je, wewe ndiye mtoto huyo?

**III. Maisha ya anasa: Luka 15:13**

Sasa alikuwa "Huru!" Alikuwa na uwezo wa kufanya kila jambo alilokuwa akitaka.
Baadhi ya watoto wa Mungu waliopo hapa usiku wa leo wameishi maisha ya ukaidi na uasi. Je, wewe ni mtoto huyo? Ushauri wa Mungu unapatikana katika 1 Yohana 2:15

**IV. Hali ya uhitaji: Luka 15:14**

Kamba ndefu imefikia mwisho wake! Siku moja ya kutisha hakuweza kulipa maana fedha zilikuwa zimeisha. Alivuta sigara yake ya mwisho, akanywa kinywaji chake cha mwisho. Siku hiyo alicheza kwa mara ya mwisho, akalala na msichana kwa mara ya mwisho. Fedha zilipoisha, wasichana nao wakaisha! Fedha zilipoisha, marafiki nao wakaisha! Rafiki zangu siku moja kama hiyo ya huyo kijana, nguvu zako zitaisha, uzuri wako utaisha, fedha zako zitakuwa zimeisha, na umaarufu wako utaisha. Ni nini kitakachofuat?

**V. Kulisha nguruwe: Luka 15:15**

Alianza kuzunguka akitafuta ajira. Mwishowe alipata – kulisha nguruwe! Hao viumbe wachafu, yeye ndiye awalinde na kuwalisha! Zaidi ya hapo, sasa tumbo ilidai, alisikia njaa! Tumbo lilikuwa tupu, akiwaangalia nguruwe wakila uzalendo ulimshinda. Sasa alikuwa tayari kula mabaki ya chakula cha nguruwe! Siyo kudhalilika huko! Nguruwe walikuwa na nafasi nzuri kuliko huyu kijana, kwa sababu walikuwa na chakula. Kijana hakuwa na chakula!

**Kwa nini lakini?** Kwa sababu nguruwe walikuwa chini ya bwana wao, lakini huyu kijana alikuwa ametanga mbali kutoka kwa baba yake. Inawezekana kuna mmoja wetu hapa usiku wa leo yupo katika dhambi, akiwa mtupu na mwenye njaa, katika maumivu na mpweke. Akiwa mbali sana kutoka kwa baba yake mwenye upendo. Je wewe ndiye huyo mtoto usiku wa leo?

**B. HATUA TANO ZA KURUDI**

Ninafurahi kwamba huo siyo mwisho wa kisa hiki! Baada ya kupitia hatua tano za kushuka, alianza kupanda hatua tano kupanda juu.

**I. Kujitambua: Luka 15:17**

"Alipozingatia moyoni mwake …" Kwa hiyo muda wote huo hakuwa katika utimamu wa akili zake! Kila mmoja anayetanga kutoka kwa upendo wa baba yake ni punguani kiroho.
Usiku wa leo sauti kutoka mbinguni inasema kuwa "Tulia, rudi katika utimamu wa akili zako."

**II. Maono: Luka 15:17**

Sasa anakumbuka kusema maneno haya, “Baba yangu!”
Ghafla akapata maono mapya! Akaanza kuona taswira ya wazazi wake. Baba yake hakua tena mkandamizaji, bali alikuwa mtoaji na baba mwenye upendo. Hilo ndilo lililo hitaji letu kubwa usiku wa leo – kupata taswira mpya ya Mungu! Yeye siyo hakimu katili mwenye hasira. Yeye ni baba mwenye upendo – “Ni Baba yangu.” Amri zake zote sheria za upendo!

**III. Uamuzi: Luka 15:18**

Ndipo alipoamua na kusema, “Nitaondoka…” Usiku wa leo unahitaji kuamua na kusema, “Nitarudi kwa Baba yangu mwenye upendo.”

**IV. Ungamo la aliyetubu: Luka 15:18, 19**

Sasa yuko tayari kuungama dhambi zake. “Baba, nimetenda dhambi. Ninaomba unisamehe.” Sasa hasemi tena kuwa, “Baba, nipe sehemu ya mali inayoniangukia!” Bali anasema kuwa “Nifanye kuwa…”

**V. Matendo: Luka 15:20**

Alikoma kuzungumza, alikoma kudhania, alikoma kuamua, na alianza kuweka katika utendaji. Alifahamu alichokuwa akitaka kutenda. Kwa hiyo aliondoka na kufanya hicho aichokuwa akitaka kufanya. Usiku wa leo unafikiri Mungu anatazamia kwamba utafanya nini? Hebu tusome jibu katika Matendo 22:16 Kwa hiyo aliondoka na kufanya hivyo! Njoo karibu hapa kwenye madhabahu usiku wa leo!